# LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar es Salaam, Tanzania
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz


## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO MUHIMU YALIYOWASILISHWA NA TUME YA HAKI JINAI KWA MHE RAIS SAMIA SULUHU HASSAN

### A. Ndugu wanahabari

Tarehe 13 Januari 2023 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Samia Suluhu Hassan alizindua Tume ya kuangalia jinsi ya kuboresha Taasisi za Haki Jinai nchini chini ya mwenyekiti wake Jaji Mkuu Mstaafu wa Tanzania Mhe Mohamed Chande Othuman. Kwa mujibu wa hadidu za rejea taasisi zilizotakiwa kufanyiwa tathimini ni pamoja na, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU), Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya Tanzania, na Ofisi ya Mashitaka Tanzania.

Tume ilianza kazi rasmi tarehe 1 Februari 2023 na tarehe 15 Julai 2023 Tume ikawasilisha taarifa yake kwa, Mhe Rais, kazi iliyochukua takribani miezi mitano(5).

Kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa na mwenyekiti wa Tume alianisha kuwa Tume ilipokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali na kuyafanyia uchambuzi na imekuja na mapendekezo ya namna ya kufanya maboresho katika taasisi hizo. LHRC inapenda kupitia mkutano huu na waandishi wa habari kuendelea kufanya uchambuzi na kuwasilisha mapendekezo ya utekelezaji kama ifuatavyo.

### B. Upelelezi na Uchunguzi

**Ndugu wanahabari**

Kwa muda mrefu LHRC imekuwa ikipigania uwepo wa mfumo huru na unaojitegemea juu ya uchunguzi na upelelezi wa makosa ya jinai hapa nchini kutokana na ukweli kwamba mfumo wa sasa kuwa sehemu ya jeshi la Polisi kitendo kinachopelekea uwepo wa uwezekano wa watuhumiwa

kubambikiwa kesi na wakati mwingine kuharibiwa au kuingiliwa kwa Ushahidi na upelelezi kuchukua muda mrefu. Hili ni moja ya pendekezo la LHRC lilitolewa kwa Tume.

LHRC inaishauri Serikali kutekeleza pendekezo la Tume la kuanzisha la kuanzishwa kwa Mamlaka mpya na huru ya inayojitegemea itakayojulikana kama Ofisi ya Taifa ya Upelelezi (OUT) yaani (**National Bureau of Investigation**) itayakoyakuwa na mamlaka ya kupeleleza kesi zote za jinai, LHRC inapendekeza kupelekwa kwa mswaada wa Sheria ya kuanzishwa kwa chombo hiki angalau Bunge la mwezi Septemba 2023 ili kurahakisha kwa ufanisi wa mfumo wa upelelezi na uchunguzi hapa nchini.

### C. Dhamana

**Ndugu wanahabari**

LHRC imekuwa ikipigania kwa muda mrefu sasa juu ya Mahakama kupewa mamlaka ya kufanya uamuzi wa ni mazingira gani mtuhumiwa apewe dhamana na ni mazingira gani yatapelekea mtuhumiwa kunyimwa dhamana tofauti na dhana ya sasa ambapo sheria ndio inayoainisha ni makosa gani yenye dhamana na ni makosa gani yasiyo na dhamana chini ya kifungu cha 148(5) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai Sura ya 20 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

LHRC ilitoa ushauri wa aina hii kupitia utafiti wake ilioufanya mwaka 2021 uliojulikana kama ***the study of unbailable offences 2021*** **kwa kuangalia suala la dhamana kwa nchi jirani kama Kenya, Uganda, Malawi, Zambia na Zanzibar ( kwa mfano, Zanzibar wana mfumo tofauti wa haki jinai na ule wa Tanzania bara)** ambapo pamoja na mambo mengine utafiti huo ulipendekeza makosa yote kama ilivyo kwa baadhi ya nchi jirani yawe na dhamana na pale mtu anaponyimwa dhamana iwe ni uamuzi wa Mahakama kulingana na aina na mazingira ya kosa tajwa.

LHRC inapendekeza kupelekwa kwa mswaada wa Sheria ya Dhamana (**Bail Act**) kama ilivyopendekezwa na Tume ili kutoa mwanya kwa masuala yote

yanayohusu dhamana kuwa chini ya sheria moja tofauti na sasa ambapo suala la dhamana linaongozwa na sheria tofauti tofauti kulingana na kosa husika, kwa mfano, Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai Sura ya 20 kifungu cha 148(5) kinachoshughulika na dhamana, Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200 ina kifungu cha 36, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Madawa ya Kulevya Sura ya 95 kifungu cha 29, Sheria ya Polisi na Polisi Wasaidizi Sura ya 322 ina kifungu cha 31.

LHRC inaishauri Serikali kuyafanyia kazi mapendekezo haya kutokana na ukweli kwamba tayari uamuzi wa aina hii ulikwisha tolewa na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu katika shauri la **Legal and Human Rights Centre & Another dhidi ya Serikali ya Tanzania maombi Na. 039/2020** uamuzi wa tarehe 13 Juni 2023. Katika shauri hili Mahakama iliagiza Serikali ya Tanzania kukifanyia marekebisho kifungu cha 148(5) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai kwa hoja kwamba kinakiuka Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu 1981 pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977.

### D. Adhabu ya Kifo

**Ndugu wanahabari**

Eneo jingine mhimu ambalo LHRC inaishauri Serikali kulifanyia marekebisho ni lile la adhabu ya kifo. Kwa mujibu wa Tume, adhabu ya kifo ni adhabu katili, inayotweza utu wa mtu na iliyo kinyume na haki za binadamu hivyo inapaswa kutokuwa adhabu ya lazima na ikitokea mtu akahukumiwa adhabu ya kifo ikapita miaka mitatu Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hajaidhinisha kunyongwa basi adhabu hii itengeuke na kuwa kifungo cha Maisha.

LHRC kwa miaka mingi imekuwa ikiishauri serikali kuridhia mkataba wa nyongeza wa kimaitaifa wa haki za binadamu wa kufuta adhabu ya kifo. Hii ni kutokana na ukweli kuwa adhabu yenyewe imedhibitika hata na Tume yenyewe mbali na madhara yake haitekelezeki. ***Mbali na Tume kusita kupendekeza adhabu hii ifutwe moja kwa moja LHRC bado***

***inapendekeza adhabu hii ifutwe***. Kwenye mfumo wa haki jinai ulio na changamoto nyingi kama zilivyoainishwa ni rahisi kumhukumu mtu adhabu ya kifo asiyekuwa na hatia.

Pamoja na LHRC kuamini kwamba adhabu ya kifo iko kinyume na misingi ya Haki za Binadamu, hata Mahakama za kikanda zilikwisha toa msimamo juu ya adhabu ya kifo, kwa mfano, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwenye shauri la **Ally Rajabu na wenzake dhidhi ya Serikali ya Tanzania maombi Na.007/2015 na la Marthine Christian Msuguri dhidi ya Serikali ya Tanzania maombi Na. 052/2016** ambapo Mahakama kwa nyakati tofauti ilitamka kuwa adhabu ya kifo***(Mandatory death penalty)*** inakiuka Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu 1981, hivyo kuitaka serikali kukifanyia marekebisho kifungu cha 197 cha Kanuni ya Adhabu Sura ya 16.

**E. Utitiri wa Vyombo vyenye Taswira ya Kijeshi**

**Ndugu wanahabari**

LHRC kwa miaka mingi imekuwa ikipiga kelele kuhsu ukatili wa majeshi haya hususani yale yanayoshughulika na wanyamapori na hifadhi zetu na kwa bahati nzuri Tume imelibaini na kutoa mapendekezo yake ni uwepo wa utitiri wa vyombo vyenye taswira za kijeshi na wakati mwingine kumiliki mahabusu ambazo hazijulikani zilipo. Kwa mujibu wa Tume, imebaini uwepo wa takribani taasisi 18 zinazofanya kazi kama Polisi wakati hazina weledi wa kufanya hivyo. Kutokana na taasisi hizo kutokuwa na weledi pamoja na mafunzo ya kutosha juu ya dhana ya ukamataji siku za hivi karibuni tumeshuhudia uvunjifu mkubwa wa Haki za Binadamu unaofanywa na maofisa wa jeshi usu lililo chini ya TANAPA, TAWA, TFS pamoja na mamlaka nyinginezo zinasosimamia mapori tengefu ikiwemo mauji na wakati mwingine mapigano kati ya majeshi hayo na wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi.

LHRC inaishauri Serikali kurudisha majukumu yote ya ukamataji mikononi mwa Jeshi la Polisi huku taasisi nyingine zilizoundwa kwa mujibu wa sheria kama vile TAKUKURU ambazo kwa namna moja ama nyingine zina mamlaka ya kufanya uchunguzi na ukamataji kufanya hivyo kwa kushirikiana na Jeshi

la Polisi pale zinapotekeleza majumu yake ya kioparesheni. Pendekezo hili halihitaji bajeti bali ni suala la serikali kufanya uamuzi.

**F. Kuanzishwa kwa Chombo Huru kitakachoghulika na Malalamiko ya Wananchi kuhusu vitendo vya baadhi ya Askari wa Jeshi la Polisi kutoenenda kwa mujibu wa sheria**

**Ndugu wanahabari**

LHRC imekuwa ikipigania uwepo wa chombo huru yaani *(**Police Oversight Body**)* kitakachoghulika na malalamiko ya wananchi juu ya baadhi ya vitendo vya askari wa jeshi la polisi kutoenenda kwa mujibu wa miongozo, kanuni, taratibu na sheria tofauti na sasa ambapo mwananchi akiwa na malalamiko juu ya Polisi anayawasilisha kwa mkuu wa Polisi wilaya au kamanda wa Polisi Mkoa kitendo ambacho kinaenda kinyume ya misingi ya utoaji haki isemayo huwezi kuwa jaji wa kesi yako mwenyewe. LHRC ilifikia mpaka hatua ya kuandaa mswaada wa mfano ambao tuliuwasilisha mbele ya Tume kama sehemu ya mapendekezo yetu.

Hata hivyo, Tume imekuja na maoni mbadala juu ya pendekezo hili ambapo Tume imependekeza chombo hiki kiwe sehemu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora yaani divisheni maalum itakayohusika na malalamiko ya wananchi juu ya vitendo vya baadhi ya askari Polisi kutoenenda kwa mujibu wa sheria. LHRC inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba chombo hiki kinapewa bajeti ya kutosha ili kiweze kushuka mpaka ngazi ya wilaya. LHRC pia inapendekeza chombo hiki kijengewe uwezo ikiwa ni pamoja na kutembelea nchi mbalimbali kama Kenya na Afrika ya Kusini kuona namna wenzao wanavyofanya kazi.

**G. Mwenendo Kabidhi (Committal Proceedings)**

**Ndugu wanahabari**

Moja ya eneo ambalo pia limeonekana kuwa na changamoto kubwa katika mnyonyoro mzima wa haki jinai ni mwenendo kabidhi ambapo makosa yote yanaysikilizwa na Mahakama Kuu, kwa mfano kosa la mauaji, makosa ya utakatishaji fedha na makosa ya uhujumu uchumi kwa mujibu wa kifungu cha 36 cha Sheria ya Uhujumi Sura 200 kama ilivyofanyiwa Marejeo mwaka

2022 na kifungu cha 243 hadi 251 vya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai Sura ya 20 kama ilivyofanyiwa Marejeo mwaka 2022 vyote kwa pamoja vinaweka ulazima wa makosa yanayosikilizwa na Mahakama Kuu kuanzia mahakama za chini yaani (committal proceedings).

Kiutaratibu wakati wa *committal* mtuhumiwa huwa haruhusiwi kusema chochote kutokana na ukweli kwamba Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi zinakuwa hazina mamlaka ya kusikiliza kosa husika hivyo shauri hupelekwa katika Mahakama hiyo kwa ajili ya Jamhuri kukamilisha upelelezi wake ambapo mtuhumiwa hupewa nakala ya vielelezo ambavyo Jamhuri itavitumia wakati wa usikilizwaji wa shauri husika. Wakati mwingine kesi huchukua miaka minne hadi mitano wakati wa *committal* huku mtuhumiwa akisota mahabusu baadae shauri hilo kuwasilishwa Mahakama Kuu ambayo ndo Mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza shauri hilo.

LHRC inaishauri Serikali kuifanyia marekebisho Sheria ili kuweka ukomo wa muda wa upelelezi, kupunguza idadi ya makosa yanayosikilizwa na Mahakama Kuu, Mkurugenzi wa Mashtaka kuondolewa madaraka ya kuipa mahakama nguvu ya kusikiliza shauri. Haya madaraka ya mkurugenzi wa mashtaka kuamua shauri lipi lisikilizwe na mahakama za chini linakiuka Katiba kwani anaweza kuingilia uhuru wa mahakama.

**Hitimisho**

Mwisho, LHRC inapenda kutoa wito kama ifuatavyo

i. Vyombo vinavyohusika na haki jinai nchini vianze kutekeleza mapendekezo ya Tume hasa yale yasiyohitaji matumizi ya fedha au kubadilisha sheria. (Wabadilishe tabia)

ii. Wadau wa Haki Jinai nchini kwa kushirikiana na Serikali watoe elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutii sheria bila shuruti ili kuepuka migogoro isiyo la lazima na vyombo vya dola

iii. Taasisi zilizoguswa na mapendekezo ya Tume ziandae mpango kazi *(Action Plan)* juu ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyogusa taasisi zao.

iv. Kuwe na mfumo wa kufanya tathimini (*Monitoring and Evaluation*) juu ya utekelezaji wa mapendekezo ya Tume.

v. Serikali ipeleke miswaada ya Sheria katika Bunge la mwezi Septemba katika mapendekezo ambayo yanahitaji mabadiliko ya sheria.

**Imetolewa Dar es Salaam Na:**

**Dr. Anna Henga (Wakili)**

**Mkurugenzi Mtendaji**